

Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1, 2014 Bei Sh. 500

NDANI

KKKT yazindua mtambo
wa 1,000 wa biogesi
Kamati ya Hali ya Hewa
Kikosi Kazi cha Kituo
cha Wanawake
chazinduliwa
Kasoro za mchakato wa
Katiba Mpya zatajwa
Maaskofu wa Ujerumani
na Tanzania wakutana


Vol. 114, Toleo la 1, 2014



ISSN 0856 - 1214

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

VITABU NA MAANDIKO



Jipatie nakala ya vitabu hivi na maandiko mengine ya Dini toka Dayosisi yako au wasiliana na:

Idara ya Misioni na Uinjilisti KKKT

S.L.P. 3033

ARUSHA

Barua pepe: elcthq@elct.or.tz



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

Mhariri
Uhuru na Amani
S.L.P. 3033
ARUSHA

Barua pepe: elobulu@elct.or.tz
sms kwa Mhariri: 0754-482-285

Fungua Tovuti ya KKKT:
<http://www.elct.org/>

MHARIRI **Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
Moshi Lutheran Printing Press
S.I.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

Newspaper Design & Typesetting:
Elizabeth Lobulu

Wachangiaji wa Makala:
Mch. Christopher Mbuga
Askofu Dkt. B. K. Bagonza
Dkt. Zebadia Mmbando
Faustina Nillan
Mch. Prof. J. Parsalaw
Askofu Mteule A. Mwenda
Askofu Mteule A. Mwaipopo
Patricia Mwaike

PICHA YA JALADA:
Watoto ni zawadi ya thamani kubwa toka kwa Mungu. Wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wana thamani na haki sawa na binadamu wengine.

PICHA: © 2013 KKKT / MICHAEL SHAYO

MAONI YA MHARIRI

Tatizo la dawa bandia ni janga linalohitaji kutatuliwa haraka

Kwa kawaida madawa mengi huagizwa toka nje kwa kuwa nchi yetu hajitoshelezi kwa utengenezaji wa madawa. Kwa hiyo mtu angedhani ingekuwa rahisi kuzuia madawa bandia yasipenyezwe kwenye soko.

Kuzuia madawa bandia yasiingie wala kusambazwa kutaokoa na kulinda viwanda vyetu vya madawa nchini. Inasikitisha kwa mfano, mgonjwa aliyepimwa na kuandikiwa dawa ya malaria anapokwenda kununua anapewa madawa bandia kwa bei ile ile kama vile anavyolipa kwa dawa halali.

Kinachoshtua pia ni taarifa kwamba baadhi ya madawa halali yanayotengenezwa hapa nchini kwa ridhaa (under licence) kwa ajili ya kutibu magonjwa ya binadamu kama malaria na ya kurefusha maisha kwa wenye virusi vya UKIMWI (ARV), yako chini ya kiwango.

Hapa tunakuwa na maswali ya kujiuliza: Je, Mtanzania wa kawaida atakwenda wapi kupata dawa halali za mifugo au za binadamu? Akipata madhara kama ulemavu yeye au ndugu zake endapo mgonjwa atafariki wafanyeje? Mifugo ikifa kwa uzembe kama huo afanyeje? Dawa bandia zilizo na viatilifu vingi kuliko inavyotakiwa matokeo yake mtumiaji anawenza kupoteza maisha.

Wafanyabiashara wasiowaaminifu nchini huweka vibandiko bandia katika vifungasho kumdanganya mnunuzi. Bahati mbaya ugonjwa hauponi na baadhi ya watu wamepoteza maisha yao au mifugo yao kwa kutumia dawa bandia.

Unajiuliza kama dawa bandia zimeweza kupenya kwa 'njia za panya' je, kodi za madawa zinakusanywa ipasavyo?

Hivi karibuni kiwanda kimoja cha umma kilichoko Kibaha kilifungwa kwa muda na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa kutengeneza na kusambaza chanjo bandia ya kutibu mdondo; hivyo wafugaji wa kuku walipata hasara kwa kuwa iligundulika kwamba ilikuwa ni chupa yenye maji ya kawaida yasiyo na dawa ndani.

Dawa za kutibu malaria zina ruzuku ya Serikali na dawa za kurefusha maisha kwa wenye VVU nazo hutolewa bure au upata ruzuku. Je anayetengeneza, kusambaza na kuuza madawa bandia ana nia ya kutibu au kurefusha maisha? Baadhi ya watu wanapata upofu au vipele kwa sababu ya kutumia dawa bandia na wengine wamepwata na athari za mzio (allergy).

Mbaya zaidi, msemaji wa Shirika la Viwango nchini (TBS) alieleza hivi karibuni kwamba shirika lake limegundua katika baadhi ya dawa bandia ya malari watengenezaji kwa makusudi hawakuwa wameweka dawa, bali walijaza unga ndani yake na wakaweka vibandiko bandia vinavyoonesha ni dawa halali kumbe siyo kweli. uchuguzi wa dawa ya kwinini uligundua ilikuwa na dawa ya flagyl na chupa ya kwinini ilikuwa na klorokwini iliyoisha muda wake. Shirika limebaini asilimia 30 hadi 40 ya dawa bandia ni za malaria.

Vyombo husika vya dola viko wapi? Je, msambazaji wa dawa kama hizo ambazo hata TBS na TFDA wanazifahamu lengo ni faida tu au ana nia nyininge?

Mauaji ni tatizo la kiroho - Askofu



Askofu Emmanuel Makala,
KKKT Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa
Victoria.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) amesema jitihada zaidi za kueneza Injili vijijini zinahitajika kukomesha mauaji ya wanawake vikongwe na albino katika Ukanda wa Ziwa.

Katika mahojiano na mwandishi wa habari hizi, Askofu Emmanuel Makala, ambaye ni Mkuu wa Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, alisema hivi karibuni "matumizi ya polisi kusaka watuhumiwa na kuwafikisha mahakamani haitoshi kukabili tatizo hilo kwani chanzo chake ni ushirikina ambao unajibiwa kwa njia ya kupenyeza Injili mionganoni mwa wana jamii.

Alisema watu walio na hofu ya ushirikina wanafikia hatua ya kutowataja watuhumiwa na hata baadhi ya askari

wanaotumwa kukamata watuhumiwa hufanya kazi kwa hofu baada ya kupewa mikasa inayohusiana na ushirikina.

Akizungumza wakati wa mukutano maalumu uliofanyika Arusha mwezi Februari baina ya Maaskofu wa KKKT na Maaskofu toka Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujeruman (VELKD), Askofu Makala alisema, "jitihada ya kueneza Injili ni suluhisho katika jamii ili kila mtu aweze kuishi katika maisha yenye staha.

"Kwa sasa hakuna jitihada za kutosha kulinda wanawake vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi – albino ambao wanaishi kama wakimbizi kwa kuwindwa kama wanyama wa porini kwa imani za kishirikina." Alisema wanyama kama tembo wanapouawa tume katika ngazi mbalimbali hadi ngazi za kimataifa huundwa ili kuwalinda.

"Ingefaa tume kama hizo ziundwe kwa ajili ya vikongwe na albino wasiuawe au watoto yatima wasikose chakula wanapokuwa vituoni," alisema.

Alitoa mfano kuhusu Kituo cha Watoto Yatima Buhangija cha Kanisa Katoliki, ambacho kipo mjini Shinyanga karibu na Ofisi ya Dayosisi ya KKKT. Kituo hicho kilanza kwa ajili ya watoto yatima lakini sasa kimepokea watoto wengi albino hivyo kimekosa uwezo wa kuwatunza vizuri. Kituo kina upungufu wa fedha kwa ajili ya chakula na mahitaji mengine. Kituo kilikuwa kwa ajili ya watoto yatima wachache lakini hadi 2014 kimepokea watoto albino 260.

Alisema japo ni kituo cha Masista wa Katoliki, Dayosisi hiyo ya KKKT mara

kwa mara hupeleka misaada ya chakula na kwamba Dayosisi ina mpango wa kusaidia suala la usafi na ukarabati wa miundo mbinu kama vile vyoo na eneo la michezo ili watoto hao waweze kuishi maisha ya staha.

Dayosisi hiyo ni mionganoni mwa Dayosisi mbili za KKKT zilizozaliwa mwaka 2013. Pamoja na kufika miaka zaidi ya 123 tangu Wamisionari wa Kilutheri toka Ujeruman walete Injili nchini; bado kuna maeneo nchini Tanzania ambayo ni ya misioni, alisema.

Washiriki wa mukutano walisema "kwa kuwa kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu inabidi sote kuwatetea wanyonge kama albino na wanawake vikongwe wanaotuhumiwa uchawi kwa kuwa na macho mekundi." Albino huuawa kwa madai kwamba viungo vya miili yao vinavuta utajiri kwa njia za kishirikina.

Wanawake vikongwe wana macho mekundi kutokana na kuishi katika nyumba zisizo na madirisha na kutumia vinyesi vya wanyama kupikia chakula kutokana na ukosefu wa kuni.

Askofu Makala alitoa mfano wa mafanikio mwaka 2008 aliposhirikiana na Wainjilisti 200 kuhubiri Injili vijijini Bariadi ambapo watu wengi walikubali kubatizwa na katika eneo walikopita mauaji ya vikongwe yalipungua.

Mwaka 2012 katika Kijiji cha Idukilo katika kipindi cha wiki moja watu 1,020 walikubali kubatizwa baada ya kupokea Neno la Mungu. Kijiji cha Sanungu mwaka 2010 kampeni ya wiki moja ilizaa matunda pale watu 1,113 walipokubali kubatizwa na kijijini hapo mauaji yalitulia; alisema Askofu Makala.



Baadhi ya Maaskofu KKKT na wa Ujeruman katika mukutano wao wa siku tano uliofanyika Arusha hivi karibuni. Kushoto ni Askofu Nicolaus Nsanganelu, KKKT Dayosisi ya Mbulu; Askofu Lucas Mbedule, KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki akifuatia na Askofu Dkt. Heinrich Bedford-Strohm, Ujeruman.

Viongozi wa Makanisa dada wakutana

Ni wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na

Umoja wa Makanisa ya Kilutheri, Ujerumani

Tanzania yataka kushiriki kupeleka Injili Ulaya

NA ELIZABETH LOBULU

Uongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) umepongeza Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani (VELKD) kwa ushirikiano wao katika kueneza Injili nchini tangu Karne ya 19 mababu zao *walipopanda mbegu ya Injili*.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, alipofungua mkutano maalumu wa Maaskofu toka Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani na wa KKKT uliofanyika jijini Arusha kwa siku tano.

Alisema yapo mambo mengi yanayotuweka pamoja yanayofanya Kanisa kuwa



Toka kushoto ni Mkuu wa Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani, Askofu Gerhard Ulrich, akifuaatiwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa na Askofu Dkt. Heinrich Bedford-Strohm.

katikati ya jamii kama vile misaada inayotolewa na Makanisa ya Ujerumani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mafunzo (scholarships) kwa watumishi. Madhumuni ya mkutano

yalikuwa ni kuimarisha uhusiano baina ya makanisa ya pande hizo mbili na kuwezesha viongozi kufahamiana na kubadilishana mawazo kuhusu kazi na changamoto

katika kueneza Injili. Katika mahojiano na mwandishi wa habari hizi, Mkuu wa KKKT, alisema kikao chao kilitoa fursa ya kujadili mchango wa Tanzania na Afrika katika kueneza Injili Ulaya.



Askofu Dkt. Steven Munga, KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, akitoa mada kuhusu "Haki Ardhi na Mazingira nchini Tanzania". Alieleza kwamba nchi hupoteza fedha nydingi kwa kusafirishwa raslimali kwenda nje ya nchi kuliko fedha zinazopatikana kwa ajili ya maendeleo. Pia alieleza kuhusu uundwaji wa "Jukwaa la Ardhi Tanzania". (PICA: © 2014 KKKT/ E. LOBULU)

Upendo wa Kristo utaleta umoja na amani, Askofu Ulrich



Wajumbe 27 toka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na kutoka Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani walipokutana Arusha 19 - 25 Februari mwaka huu walipata nafasi ya kujifunza mambo kwa pamoja na walijadili mada kuhusu mambo ya kiroho, kiuchumi, mazingira na ekolojia katika nchi hizo mbili. (PICHA: © 2014 KKKT/ E. LOBULU)

Upendo wa Kristo uwe dira yetu katika kutimiza utume wa kuwahubiri na kuwashudumia watu kiroho na kimwili.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani (VELKD), Askofu Gerhard Ulrich (Kiel/Schleswig), wakati wa kufunga mkutano wa Maaskofu wa Tanzania na Ujerumani.

Alisisitiza Neno kutoka Yohana 15: 1 -11 kwamba sisi tu matawi na tu wamoja tunapokaa ndani ya Kristo. Lakini tunatoa matunda tofauti kwa kadiri ya vipawa tulivyopewa. Alimalizia kwa kusema: "Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu."

Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani uliundwa na makanisa nane ambayo pia ni wanachama wa Makanisa ya Kiinjili ya Ujerumani (EKD).

Umoja wa makanisa ya VELKD ulianza tarehe 8 Julai 1948 mjini Eisenach, Ujerumani kwa lengo la: "**kukuza na kulinda umoja katika urithi wa Kilutheri**".

Makanisa nane yanayounda VELKD ni: Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Bavaria; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Brunswick; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Ujerumani



Kushoto ni Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akiongea wakati Mkuu wa KKKT akiagana wa maaskofu wa Ujerumani katika hafla fupi hoteli ya New Safari, Arusha.

Kati (EKM - tangu Januari 2009); Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Nchi ya Hanover; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Mecklenburg; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la North Elbian; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Saxony na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Schaumburg-Lippe.

Maaskofu hao pamoja na mambo mengine walijadili mada kuhusu mambo ya kiroho, kiuchumi, mazingira na ekolojia katika nchi hizo mbili. Kutoka Ujerumani mada zilihusu utandawazi,

mazingira na haki ya ekolojia. Na kwa upande wa Tanzania mada zilihusu Mchakato wa Katiba Mpya, mauaji ya vikongwe na albino, mazingira na haki ya ardhi.

Imekuwa kawaida kwa viongozi wa KKKT kukutana na Wakurugenzi wa Misioni au Makatibu wa Idara za Afrika katika vikao nchini na hata katika ziara za nje ya nchi.

Na Kanisa linaona vema kukutana ana kwa ana na Maaskofu kwani wao ndio walio na watu, alisema Mkuu wa KKKT.

Utoto ni wakati adimu na hupita haraka sana. Ni lazima kuhakikisha unakuwa wakati wa furaha na amani. Ni jukumu la wazazi kuwajengea watoto misingi imara kwa ajili ya wakati huo na wakati ujao. Ustawi wa watoto una mchango mkubwa katika ustawi wa jamii, Kanisa na Taifa. Watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, udhalilishwaji, utelekezwaji na unyonywaji, wananyimwa fursa ya kukua na kufikia utimilifu wao.

Watoto ni zawadi ya thamani kubwa toka kwa Mungu. Wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wana thamani na haki sawa na binadamu wengine. Bwana Yesu anayajali maslahi ya watoto. Ufalme wa Mungu aliokuja kuuanzisha katika Yesu Kristo, unawahu watoto pia.

Bwana Yesu anawapenda, anawathamini, anajali ustawi wao na anakuwepo kwa ajili yao. (Mt 18: 1-7; Mt 25: 31 - 46; Mk 10: 13 - 16). Hivyo, Kanisa lina wajibu wa kutetea haki na kulinda maslahi ya mtoto. Ni lazima lifundishe na kupinga mila potofu na kandamizi zisizodumisha maslahi ya watoto.

Neno maslahi, kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ni: ***manufaa au faida aipatayo mtu baada ya kufanya biashara, kazi au kumaliza tendo lolote.*** Kwa maana nyingine, hakuna maslahi pasipo uwekezaji. Huwezi kuvuna usipopanda.

Maslahi ya watoto yanapopewa kipaumbele na wazazi pamoja na wadau wengine, utoto wa watoto wetu na kuvuka kwao kuingia utu uzima, unatokeza matunda mazuri. Wajibu huu hauna mjadala, si jambo la hiari, si kazi ya juma au muhula mmoja.

Ni wajibu wa muda wote (full time), unaodai kujitoa kwa dhati kwa ajili ya tija kwa mtoto binafsi, jamii, Kanisa na Taifa kwa ujumla. Kinyume chake, watoto watakosa haki zao, dhamira zitatushtaki, na mustakabali wa Taifa letu utakuwa hatarini.

Maslahi ya mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 29 ya 2009 ya Tanzania ni: ***Mambo mazuri, mema, yenye kumlinda, kumwendeleza na kulinda utu wa mtoto ambayo anatakiwa ayapate, afanyiwe, au yazingative kwenye mambo yote yamhusuyo.***

Haya ni lazima yapewe kipaumbele katika matendo, maamuzi yote

Wazazi wanawajibika kulinda maslahi ya watoto



Mchg. Christopher Mbuga.

yanayomhusu mtoto na ambayo yanatekelezwa na watu binafsi, mamlaka, idara, taasisi, makampuni, yanapokuwa yanatekeleza majukumu ya kila siku nchini Tanzania. Ni sehemu ya makubaliano ya haki za mtoto ya kikanda na kimataifa, ambayo nchi yetu imeyaridhia pia. Si mkakati wa kuharibu mila na desturi za Kiafrika kama wengine wanavyodai.

Sheria ya Mtoto niliyoirejea inawataka wadau wote kujali maslahi ya mtoto. Ni ukweli usiopingika kuwa mfono mmoja haulei mwana. Lakini mwajibikaji wa kwanza katika hili na mengine ni wazazi. Wao ni ‘wakurugenzi watendaji’ wa senta ya awali ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. Hapa mtoto anawezeshwa kukua na kufikia utimilifu wake katika nyanja zote za kimwili, kiakili, kiroho, kijamii, kihisia, kimaadili na kimaonzo.

Marafiki na washirika wa awali na wa karibu wa mtoto ni wazazi.

Kwa maeleo zaidi Mwandishi anapatikana kwa barua pepe:
 <christopher_mbuga@yahoo.com>

Kanisa linaleta furaha na matumaini kwa watoto



Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, Bibi Faustina Nillan akiwa na watoto walioathirika na mafuriko yaliyotokea Januari 2014. Watoto hao wanaishi katika mahema eneo la Mateteni, Dakawa, Morogoro kutokana na makazi yao ya awali kuharibiwa na mafuriko.

Kanisa liliwapa msaada wa nguo, viatu, sabuni, mafuta na dawa za meno mnamo tarehe 22 Machi 2014.

Ni Askofu Mwenda Dayosisi ya Ruvuma

Dayosisi ya Ruvuma inayoandaliwa kuwa dayosisi ya 23 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) inatarajiwa kuzinduliwa 27 Julai mwaka huu siku ambayo viongozi wa dayosisi watawekwa wakfu.

Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Dayosisi hiyo ulifayika Msamala mjini Songea tarehe 29 Januari mwaka huu ambapo Mch. Amoni Joel Mwenda aliteuliwa kuwa Askofu na Mch. Lawrence Ng'umbi alichaguliwa kuwa Msaidizi wa Askofu.

Mch. Mwenda alizaliwa Kidegembye Wilaya ya Njombe tarehe 28 Oktoba 1966 na kubarikiwa kuwa Mchungaji 13 Novemba 2009 Usharika wa Songea Mjini. Mch. Mwenda alikuwa Mchungaji Sharika za Msamala, Songea, Mbamba-bay na Mbinga.



Mch. Amoni Joel Mwenda, (Askofu Mteule) wa KKKT Dayosisi ya Ruvuma (inayoandaliwa).

wa Elimu ya Kikristo Dayosisi ya Konde na Mchungaji katika Sharika za Dayosisi hiyo.

Mch. Mwaipopo ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Gettysburg, Marekani alikotunukiwa Shahada ya Uzamivu katika Theologia (Master of Sacred Theology) mwaka 1994 baada ya kuhitimu Shahada ya Mambo ya Dini (Bachelor of Divinity) mwaka 1992 na Cheti cha Theolojia mwaka 1985 toka Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira wakati huo kilijulikana kama Chuo cha Theolojia. Pia mwaka 2008 Mch. Mwaipopo alihitimu Shahada ya Uzamivu ya Utawala wa Biashara (MBA) toka Chuo cha Menejimenti Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI), Arusha.

Mwaipopo awa Askofu

Mkutano Mkuu Maalum wa KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika (inayoandaliwa), uliofanyika Sumbawanga tarehe 10 - 11 Januari mwaka huu pamoja na mambo mengine, ulifanya uchaguzi wa Askofu na Msaidizi wake.

Viongozi waliochaguliwa ni Mch. Ambele Anyigulile Mwaipopo, Askofu Mteule na Mch. David Masaoe, Msaidizi wa Askofu.

Kabla ya hapo Mch. Mwaipopo alikuwa Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT tangu mwaka 2000. Mch. Masaoe alikuwa Mchungaji katika Sharika za Dayosisi hiyo.

Akitoa taarifa kwa watumishi, *Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala KKKT, Bw. Abel Mrema*, alisema: "Tuwakumbuke Mch. Mwaipopo na Mch. Masaoe katika sala zetu kwa wajibu mkubwa waliopewa na pia kuombea watumishi na Washarika wote wa Dayosisi hiyo mpya ipate kusimama na kutembea kama mpango wa Mungu kwa Kanisa letu."

Watumishi wengine wa Ofisi Kuu ya KKKT nao walisema: "Nampongeza Mch. Mwaipopo katika

nafasi hiyo mpya ya utumishi. Namshukuru Mungu pia kuwa

katika ofisi yetu ameonekana mtumishi wa Bwana. Mungu atusaidie sote tuweze kumpa ushirikiano unaohitajika,"

Mwl. William Kivuyo, Kitengo cha Elimu KKKT.


"Namtukuza sana Mungu kwa matendo makuu haya. Mungu ampe mtumishi wake Mch. Mwaipopo nguvu, hekima, na busara kuitenda kazi hiyo kubwa na nzito. Kwangu mimi wajibu na nafasi hiyo ni matunda ya utumishi wake aliofanya shambani mwa Bwana kwa miaka mingi,"

Felix Mweta, Ofisi ya Hazina, KKKT.

"Baba Askofu Mteule, hongera sana. Munguakuwezeshe katika utumishi huo mpya. Amani ya Bwana itawale," *Mch. Anicet Cornel Maganya, Dawati la Utetezi KKKT.* "Munguaendelee kukuongoza, tunakupongeza na pia kukupa pole kwa majukumu yatakayo kuwa mbele yako," *Bibi Faustina Nillan, Kurugenzi ya Wanawake KKKT.*

Dayosisi hiyo iliyoko katika mikoa ya Rukwa na Katavi itazinduliwa na viongozi wake kuwekwa wakfu mwezi Septemba mwaka huu.

Aliwahi kuwa Katibu wa Misioni na Uinjilisti na Katibu



Kushoto Mch. Ambele Mwaipopo, (Askofu Mteule) wa KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika akifuatiwa na Askofu Charles Rabson Mjema wa KKKT Dayosisi ya Pare.

Mkutano Mkuu wa Wanawake KKKT kufanyika Kibaha

NENO KUU: “*Angalia, ukatulie usiogope wala usife moyo,*” Isaya 7: 4

Dayosisi ya Mashariki na Pwani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) itakuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Wanawake KKKT unaotarajiwa kufanyika tarehe 9 mpaka 13 Julai mwaka huu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkuza, Kibaha.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Kanisa KKKT.

Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, Bibi Faustina Nillan alisema hivi karibuni kwamba Halmashauri ya Wanawake iliyokutana Arusha hivi karibuni iliweza kuandaa ajenda na matukio mengine ya mkutano.

Pamoja na kupokea ripoti ya utendaji na kujadili. Wajumbe watapokea na kujadili mada na kutakwa na agenda kuhusu harambee kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Wanawake KKKT kinachotarajiwa kujengwa Kijiji cha Chilungulu, Wilayani Bahi, Dodoma.

Tarehe 16 Novemba 2013 Mkuu wa Dayosisi ya Dodoma, Askofu Amon Kinyunyu, alikabidhi rasmi mradi wa maji kijijini hapo Chilungulu ambapo ilikuwa ni ahadi ya Kanisa kwa kupewa eneo la kituo cha wanawake.

Mwezi huo Novemba Makatibu wa Idara za Wanawake toka Dayosisi za KKKT walihudhuria warsha kuhusu “Utatuza wa Migogoro kwa Amani

Makatibu wa Idara za Wanawake KKKT wakiwa katika Mkutano wa Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Wanawake. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wanawake Bibi Monica Ngavatula.



Endelevu.” Washiriki walipata fursa kushuhudia makabidhiano ya mradi wa maji na kutembelea eneo la Chilungulu. Waliweza kupanda miche kadhaa ya minyaa katika mipaka ya shamba hilo lenye ekari 296.4.

Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi walilishukuru Kanisa kwa kushirikiana nao katika kutatua tatizo la maji katika Kijiji cha Chilungulu. Shukrani hizo zilitolewa na Msaidizi wa Mhandisi wa Maji Wilaya ya Bahi Bw. Mathias Buhoro aliyeshuhudia makabidhiano ya Mradi wa Maji wa Chilungulu.



Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi walilishukuru Kanisa kwa kushirikiana nao kutatua tatizo la maji katika Kijiji cha Chilungulu. Pichani ni Msaidizi wa Mhandisi wa Maji Wilaya ya Bahi, Bw. Mathias Buhoro, akimpa mkono Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, Bibi Faustina Nillan.

PICHA: © 2014 KKKT- KURUGENZI YA WANAWAKE / MCHG. MIMII BROWN.

Atoa wito kuombea Mkutano


Mkurugenzi wa Kazi za Wanawake KKKT, Bibi Faustina Nillan, ametoa wito kwa washarika na wadau wengine kuomba kwa ajili ya mkutano ujao wa wanawake.

Mkutano huo utaongozwa na Neno Kuu: “*Angalia, ukatulie usiogope wala usife moyo,*” (Isaya 7: 4).

Baadhi ya mada ni pamoja na ‘*Elimu ya Afya ya*

Mwanamke (Saratani ya Matiti na Shingo ya Kizazi); ‘Utandawazi na Malezi ya Watoto’; ‘Wanawake na Uongozi’ na ‘Usuluhishi wa Migogoro’.

Mkuu azindua kikosi kazi kwa ajili ya kituo cha wanawake



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa akizindua 'Kikosi Kazi kwa ajili ya kuendeleza Kituo cha Wanawake KKKT' kinachotarajiwa kujengwa Mkoani Dodoma.

Wajumbe wa Kikosi Kazi hicho ni pamoja na Mhe. Mercy Silla, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga; Bw. Shedrack Kitomari, Meneja wa NSSF Mkoa wa Manyara na Bw. Julius Mosi, Katibu Mkuu KKKT Dayosisi ya Kaskazini. Wengine ni Bw. Titus Ngwatu, Mfanyabiashara jijini Arusha na Bw. Theophilus Kahigwa, Mkurugenzi wa Active KMK.



Makatibu wa Idara za Wanawake Dayosisi za KKKT wakiwa katika eneo linalotarajiwa kujengwa Kituo cha Wanawake walifanya maombi na kupanda minyaa kwenye uzio.



Halmashauri ya Wanawake iliyokutana Arusha mwaka huu pamoja na mambo mengine ilijadili agenda za kuwekwa kwenye mkutano mkuu.

Wanawake washauriwa kutokata tamaa



Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, Mchg. Rachel Axwesso, (aliyesimama) alimkaribisha Mkuu wa KKKT kuzindua Kikosi Kazi kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Wanawake KKKT tarehe 7 Aprili mwaka huu. Wa pili kulia ni Bw. Abel Mrema Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala, KKKT.

Mkuu wa KKKT alisema katika hafla

hiyo fupi kwamba ametiwa moyo kwa viongozi wa Kurugenzi ya Wanawake KKKT kuonesha nia ya kutekeleza mpango wa kuwa na kituo kwa ajili ya maendeleo ya wanawake na Kanisa kwa jumla.

Alitaka tathmini ya Kikosi kazi hicho ifanyike baada ya mwaka mmoja kuona kama kinatimiza wajibu wake. Alisema naye angependa kuwa bega kwa bega

na kikosi kazi hicho. Pia alitoa mifano mbali mbali kuwatia moyo wanawake wasikate tamaa kirahisi katika kufuatilia na kutekeleza majukumu yao. Na aliahidi Kanisa lipo tayari kusaidia ili kituo kiweze kukamilika.

Alitoa wito watendaji wahakikishe wanakwenda vyombo husika kufuatilia ili kupata hati ya kumiliki ardhi mapema iwezkanavyo.



Mwenyekiti wa Wanawake KKKT, Bibi Monica Ngavatula (kushoto), akipanda mmea wa mnyaa hivi karibuni kwenye uzio wa eneo la Kituo cha Wanawake KKKT kinachotarajiwa kujengwa katika Kijiji cha Chilungulu -Bahi, Dodoma.

PICHA: © 2014 KKKT - KURUGENZI YA WANAWAKE / MCHG. MIMII BROWN.



Katibu wa Idara ya Wanawake Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria, Mchg. Mimii Brown akiwa na watoto wa Chilungulu hivi karibuni.

KKKT yazindua mtambo wa 1,000 wa ‘biogesi’


Mratibu wa Programu ya Uhai na Mazingira Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bibi Patricia Mwaikenda, amesema hivi karibuni kwamba Kanisa limekwisha zindua mtambo wa 1,000 wa ‘biogesi’ nchini.

Alisema ‘biogesi’ ni ukombozi kwa familia kwa kuwa nishati hiyo hurahisisha kazi ya kupika na kuondoa ghamama ya kuwasha taa. Wasichana na wanawake ambao hutafuta kuni baada ya kupata mtambo wa “biogesi” wanapata muda zaidi wa uzalishaji mali.

Akitoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alisema tangu mtambo wa kwanza uzinduliwe na Askofu Job Mbwiwa wa KKKT Dayosisi ya Kusini Magharibi 2010 Kanisa limesambaza kwa kasi mitambo hiyo.

Askofu Michael Adam wa KKKT Dayosisi Mkoani Mara akizindua mtambo wa 1,000 wa ‘biogesi’ Jimbo la Serengeti.

PICHA: © 2014 ELCT-SLEP / P. MWAIKENDA




Askofu Mbwiwa akizindua mtambo wa kwanza wa ‘biogesi’ ulifungwa nyumbani kwa Bw. Onesta na Bibi Nisamehe Sanga.



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa alizindua mtambo wa 800 ulifungwa nyumbani kwa Bw. na Bibi Joshua Mwanga- Makumira, Arusha.

Mtambo wa 1,000 ulizinduliwa Jimbo la Serengeti na Askofu wa Dayosisi Mkoani Mara Michael Adam tarehe 22 Desemba mwaka jana. Pia wakazi wa Kijiji cha Saguti Wilaya ya Musoma vijijini waligaiwa ng’ombe wa maziwa 20 na vifaa vya kuchemsha maji ya kunywa 40 vyenye ujazo wa lita 10.



Mratibu wa Programu ya Uhai na Mazingira Patricia Mwaikenda (kulia) akiwa na Mhasibu wa Programu hiyo Bibi Elihuruma Machange.

KKKT yakaribisha Jubili ya Mkutano wa Marangu

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linakaribisha matukio ya kumbukumbu ya Jubili ya miaka 60 tangu Mkutano wa Viongozi wa Makanisa barani Afrika ulipofanyika Marangu, Mkoani Kilimanjaro; ambapo ilikuwa ni mara ya kwanza kwa viongozi wa makanisa ya Kilutheri barani Afrika kukutana.

Akizindua kamati ya maandalizi iliyokutana Moshi Mkoani Kilimanjaro hivi karibuni, Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) Kanda ya Afrika alisema: “*Mkutano wa Marangu ulikuwa wa kihistoria na ufumbuzi kwa masuala ya umoja, heshima, msimamo, uhuru wa kujiongoza na maendeleo ya makanisa barani Afrika.*”

Mkutano wa kamati hiyo uliratibiwa na Dawati la Afrika la FMKD ili kupendekeza ajenda, mada, washiriki na bajeti ya matukio ya *Jubili ya Mkutano wa Marangu* yatakayofanyika mwaka ujao.

Askofu Malasusa alisema katika mkutano wa mwaka ujao, “FMKD limeipa fursa Kanisa bara la Afrika kutoka na ajenda za kujadiliwa wakati wa maadhisho ya kimataifa kukumbuka miaka 500 ya *Matengenezo ya Kanisa* yatakayofanyika Windhoek, Namibia mwaka 2017.”

Katibu wa Dawati la Afrika FMKD, Mch. Dkt. Elieshi Mungure alisema kamati ilipendekeza mkutano wa viongozi na matukio mengine kwa ajili ya *Jubili ya Mkutano wa Marangu* vifanyike mjini Moshi na Ibada siku ya kilele ifanyike Jumapili huko Marangu.

Dkt. Mungure alisema mapendekezo ya kamati yatapelekwa mbele ya kikao cha Halmashauri Kuu ya



Askofu Mstaafu Dkt. Zephania Kameeta wa Namibia.

FMKD itakayokutana hivi karibuni kupata kibali.

Askofu Mstaafu Dkt. Zephania Kameeta wa Kanisa

la Kilutheri Namibia aliyekuwa Mwenyekiti wa kikao cha maandalizi kilichofanyika tarehe 25 - 27 Machi mwaka mjini Moshi huu ailezea:

“Washiriki wa kikao cha Marangu mwaka 1955 walienda huko mioyo yao ikiwa mizito kwa kuwa nchi zao zilikuwa chini ya ukoloni.

“Kulikuwa na ari ya kutaka kujitawala na shauku ya kutaka kukomboa bara la Afrika kwa ujumla. “Mkutano wa Marangu ulikuwa muhimu sana kwa bara zima la Afrika. Na kumbukumbu yake itahuisha ari ya viongozi wa Kilutheri Afrika kuvumbua upya urithi wetu.”

Viongozi hao walipokutana mwaka 1955 Marangu,

Kilimanjaro walikuwa na maono ya kuwa na Kanisa linalojitegemea.

Wakati huo ni makanisa mawili tu yalikuwa wanachama wa FMKD Afrika - Kanisa la Madagaska na Kanisa la Kaskazini mwa Tanganyika kwa wakati huo.

“Kablayakwendakuadhimisha Siku ya Matengenezo kimataifa, Waafrika tutakutana kujadili namna ya kuhuishwa Kanisa barani mwetu ikiwa ni pamoja na **‘Matengezo ya Kanisa.’**”

“Mwaka 1570 Martin Luther alisema **‘Matengenezo ya Kanisa’** ni jambo endelevu. Kwa hiyo ari yetu hiyo (Waafrika) itaendelea kuwepo hata baada ya mwaka 2017,” alisisitiza.

Askofu Bagonza afanya ziara Uganda



© 2014 ELCT-KAD

Mwezi Machi mwaka huu Askofu Dkt. Bagonza (aliye na fimbo) akifuatana na Mch. Ambele Mwaipopo (Askofu Mteule Dayosisi ya Ziwa Tanganyika), alifanya ‘Ziara ya Kichungaji kwa Kanisa la Kilutheri Uganda.’ Askofu alibariki na kuwaingiza kazini Wachungaji, alibatiza watoto; alitoa Kipaimara na kufungisha ndoa. Kulia ni Mch. Elisa Bagenyi, Kiongozi wa Kanisa la Uganda. Picha kwa HISANI YA DAYOSISI YA KARAGWE

KKKT yatathmini Muundo Ofisi Kuu na kuandaa Mpango Mkakati



Baadhi ya wajumbe walioshiriki warsha iliyojadili na kuandaa rasimu ya kwanza ya Mpango Mkakati wa KKKT.

PICHA: © 2014 KKKT

KKKT ilivyochangia kukua kwa huduma ya tiba shufaa

NA DKT. ZEBADIA PAUL MMBANDO

Huduma ya Tiba Shufaa (Palliative Care) ni sehemu mojawapo ya tiba ya kisasa inayowalenga wagonjwa wenye magonjwa ya kusendeka au yale ambayo tiba yake ni ngumu au yasiyopona kirahisi. Walengwa wa aina hii ya tiba ni wagonjwa wa kansa, UKIMWI, kiharusi, magonjwa ya moyo yaliyopitiliza ukomo wa kutibika, nk.

Huduma hii pia hujulikana kama Tiba ya huruma kwa sababu lengo lake ni kumpunguzia mgonjwa maumivu ya aina zote, hata pale ambapo hatuwezi kumtibu kabisa. Ni huduma ya pekee ambayo ili kuifkisha kwa mlengwa inapaswa kujumuisha mahitaji ya mgonjwa katika ujumla wake (yaani kimwili, kijamii, kisaikolojia na kiroho pia). Huduma hii inaratibiwa na watumishi wa programu ya Tiba Shufaa (Palliative Care Program) Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na kutekelezwa na hospitali 20 za KKKT.

Katika KKKT, Huduma ya Tiba Shufaa ilianza mwaka 1999 katika Hospitali ya Kilutheri ya Selian kupitia Kitengo cha "Selian Hospice" na tangu mwaka 2004 Kanisa lilianza mipango ya kueneza katika hospitali zote. Tangu 2006 programu hiyo ilipata nguvu baada ya kupokea misaada kutoka watu wa Marekani ambapo huduma kamilifu (Holistic care) zilianza kutolewa katika hospitali zifuatazo za Kilutheri: Illembula, Bumbuli, Iambi, Marangu, Machame, Gonja na Bunda (DDH).

Miaka miwili baadaye huduma ya Tiba Shufaa ilitolewa rasmi katika hospitali sita zaidi - Itete, Matema, Nyakahanga, Ndolage, Haydom na Nkoaranga.

Miaka 10 baadaye, huduma hii ikafikia hospitali 20 za KKKT zilizoko nchi nzima, zikiwa na utaalamu wa kutoa huduma kamilifu kwa wagonjwa wenye maumivu makali na magonjwa nyemelezi yatokanayo na VVU, kansa, nk.

Malengo ya KKKT katika tiba shufaa: Awali, kuanzishwa kwa Tiba shufaa katika KKKT kulilenga sana wagonjwa na familia zilizoathiriwa na VVU na UKIMWI. Lakini huduma iliweza pia kuwfikia wagonjwa wengine ambaa mahitaji yao kiafya yaliangukia katika kundi la tiba shufaa kama wagonjwa wa kansa, nk. Aidha malengo ya Kanisa pia yalijikita moja kwa moja



Wafamasia kutoka baadhi ya Hospitali za KKKT wakiwa wamebeba dawa aina ya Morphine kwa mara ya kwanza baada ya kupata mafunzo kutoka Hospitali ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam. (PICTA: © 2014 ELCT PALLIATIVE CARE PROGRAM)

katika miongozo mbalimbali ya Biblia kama ifuatavyo:

- Elimu na uhamasishaji (Hosea 4;6): Hapa KKKT lililenga kutoa elimu kuhusu magonjwa kama VVU na jinsi ya kijikinga nayo au jinsi salama ya kuishi na magonjwa hayo ili wasiangamie.
- Ushauri na upimaji wa hiari wa VVU (Warumi 15:1) Kuonyesha mfano na njia katika kuwasaidia wale wenye matatizo magumu ya kiafya.
- Kuzuia virusi toka kwa mama kwenda kwa mtoto kama inavyooneshwa katika Isaya 65: 20 na 23.
- Huduma ya wagonjwa nyumbani kama ilivyo katika Mathayo 25: 34 - 40.
- Msaada kwa watoto yatima ilivyo katika Yakobo 1:27 na 2: 14 -17.
- Lakini pia huduma ya madawa ya kupunguza makali ya UKIMWI ilivyo elekezwa kwenye Jeremia 30: 17.
- Elimu ya afya ya uzazi na UKIMWI kwa vijana ilivyo katika Mhubiri 11: 9.
- Kuanzisha Timu za Watenda Kazi: Mpaka sasa, vyuo vingi vya mafunzo ya sayansi ya Tiba havina "Mtaala wa Tiba Shufaa", kwa hiyo, Program ya Tiba Shufaa ililazimika kutoa mafunzo (ya muda mfupi na muda mrefu) kwa wataalamu walio katika hospitali zake ili waweze kutoa huduma stahili kwa

wagonjwa husika. Hadi 2014 programu hii imeweza kufundisha **Timu za Tiba Shufaa** katika hospitali zote 20 wakiwemo madaktari, wauguzi, maofisa Ustawi wa Jamii na Wachungaji wenye uzoefu wa kutoa tiba kamilifu (Holistic Care) kwa wagonjwa wenye uhitaji huo. Ili kuanza kazi, timu hizi pia zilihitaji vitende kazi kama madawa, vyombo vya usafiri, mafunzo endelevu, nk.

Utetezi juu ya upatikanaji na matumizi ya "Morphine"

Upatikanaji wa dawa za aina ya **Morphine** ambazo hutumika kwa wagonjwa wenye maumivu makali ulikuwa mgumu kwani mpaka 2011, ni vituo vinne tu hapa Tanzania vilikuwa na kibali cha kutoa dawa hizi zikiwemo Hospitali ya **Ocean Road Cancer Institute** (DSM), **Selian Hospice** (Arusha), PASADA (DSM) na **Muheza Hospice** (Tanga). Kufuatia utetezi wa kina na ushirikiano wa karibu na taasisi za kitaifa na kiserikali kama ORCI, TPCA, TFDA na Wizara ya Afya, kwa sasa zaidi ya asilimia 90 ya hospitali za KKKT zina vibali na uwezo wa kutoa dawa ya **Morphine** kwa wagonjwa wenye maumivu makali. Kwa kuwa dawa hii ni ya bei nafuu kuliko dawa nydingi za maumivu, hii pia imesaidia kuongeza upatikanaji kwa wagonjwa wenye kipato duni.

Mchakato wa Kuandika Katiba Mpya Tanzania

NA ASKOFU DKT. BENSON BAGONZA,
KKKT DAYOSISI YA KARAGWE.


UTANGULIZI

Mchakato wa uandikaji wa Katiba Mpya nchini Tanzania, unaeleweka kwa namna mbili. Kwanza, wapo wanaoamini kuwa inaandikwa Katiba Mpya kabisa. Hata Sheria inayoongoza mchakato huu ndivyo inavyosema baada ya kuwa imefanyiwa marekebisho ya msingi.

Kundi la pili, linaamini Katiba iliyopo inafanyiwa marekebisho. Hawa wanaongozwa na uzoefu uliojitekeza pale Serikali ilipoleta Muswada wa Marekebisho ya Katiba badala ya Muswada wa Kuandika Katiba Mpya. Kuna sababu nyingi za kudhani kuwa kinachofanyika ni kurekebisha Katiba iliyopo japo sheria inayoongoza mchakato inasema itaandikwa upya.

KWA NINI KATIBA MPYA?

Kimsingi kuna sababu kuu tatu za kuandika katiba mpya. Kwanza, katiba iliyopo iliandikwa wakati wa chama kimoja lakini hivi sasa tuna mfumo wa vyama vingi. Pili, Katiba iliyopo iliandikwa wakati wa mfumo wa uchumi wa kijamaa uliomilikiwa na dola, lakini hivi sasa tuna uchumi huria unaomilikiwa na sekta binafsi tena yenye makampuni mengi ya kigeni. Tatu, Muungano katika Tanganyika na Zanzibar uliofanyika miaka 50 iliyopita unadai mtazamo mpya na kuwashirikisha watu zaidi kuliko kuujenga juu ya utashi



Askofu Dkt. Benson Bagonza,
KKKT Dayosisi ya Karagwe.

wa viongozi tu. Zipo sababu nyingine hasa zile zinazolenga kuondoa au kupunguza madaraka ya mtu au makundi fulani fulani katika jamii na kupanua wigo wa demokrasia kwa umma.

MCHAKATO WENYEWE

Mchakato wa kuandika katiba mpya kisheria una hatua nane muhimu. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kurekebisha Sheria au kutunga Sheria ya Uandikaji Katiba Mpya. Baada ya mvutano wa ama turekebishe au tuandike katiba mpya, sheria ilipelekwa bungeni na kuitishwa kuruhusu mchakato kuanza kuandika Katiba mpya. Hatua ya pili ilikuwa kuteua Tume maalumu ya Kukusanya Maoni. Hii ilijumuisha wajumbe 30 na sekretariati yake. Kila upande wa Jamhuri ulikuwa na idadi sawa ya wajumbe. Hatua ya tatu ilikuwa kwa Tume hiyo kuzunguka

nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Katiba mpya. Wapo walioongea mbele ya Tume, wengine waliandika na wengine kutuma ujumbe kwa njia ya simu.

Hatua ya nne ilikuwa ni kwa tume kukaa chini na kuandika Rasimu ya Kwanza ya Katiba. Ndipo katika hatua ya tano, rasimu hiyo ilitumwa katika mabaraza ya Wilaya yenyewe wajumbe kutoka Kata zote nchini ili ijadiliwe. Mabaraza haya yalichaguliwa na wananchi katika Kata na wawakilishi wake kwenda Wilayani kujadili rasimu.

Maoni yaliyokusanya kutoka mabaraza ya Wilaya, katika hatua ya sita, yalipelekwa mbele ya tume na tume ikaandika Rasimu ya Pili ya Katiba na ilikabidhiwa kwa Rais.

Katika hatua ya saba, makundi mbalimbali yalituma mapendekezo kwa Rais ili aweze kuteua Wabunge wa Bunge Maalum la Katiba. Bunge hilo lina wajumbe kutoka makundi makubwa matatu yaani: Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi (Zanzibar) na kundi la wajumbe 201 walioteuliwa na Rais kuwakilisha makundi mbalimbali ya kijamii hapa nchini. Makundi haya ni kama yale ya wana taaluma, mashirika ya kidini, wana harakati, wakulima, wafugaji, walemovu na wengine. Bunge hili lina wajumbe zaidi ya 600 na linatakiwa kujadili na kuboresha rasimu ya pili ya Katiba na ndipo utaingia katika hatua ya nane ya Upigaji Kura ya Maoni (Referendum). Kura hii itapigwa nchini kote kuitisha au kukataa Katiba Mpya.

Masuala tete katika kuandika Katiba Mpya

Pamoja na mijadala mingi inayoendelea katika Taifa letu kuhusu uandikaji wa Katiba Mpya, yako mambo saba yaliyoibua hisia yalipojadiliwa:

- Muungano na muundo wake:** Wako wanaopendekeza muungano wa Serikali moja, mbili, tatu na wengine wanapendekeza muungano wa mkataba.
- Dini ya Dola:** Upo mvutano wa ama Serikali iwe na dini rasmi au isiwe na dini. Hii ni pamoja na uwepo au kutokuwepo kwa mahakama za kidini hapa nchini.
- Ukomo wa muda wa mtu kuwa Mbunge:** Rasimu inapendekeza vipindi vitatu vya ubunge yaani miaka 15.

- Uteuzi wa watendaji:** Kupunguza madaraka ya Rais katika kuteua watendaji mbalimbali Serikalini na badala yake kushauriwa na vyombo fulani au hata uteuzi wake kuidhinishwa na vyombo vingine.
- Madaraka ya kumwondo Mbunge:** Madaraka ya wananchi kumrejesha au kumwondo Mbunge wao kabla ya wakati endapo hawawakilishi vizuri.
- Mamlaka ya Bunge kumwondo Rais:** Bunge kupewa madaraka ya kumrejesha au kumwondo Rais endapo atafanya makosa makubwa.
- Haki za binadamu:** Haki za binadamu kutambuliwa rasmi Kikatiba.

Askofu Dkt. Benson Bagonza alitoa mada hili kwa mara ya kwanza Maaskofu wa KKKT walipokuwa na kikao cha pamoja cha mashauriano na Maaskofu wa Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani (VELKD). kilichofanyika Hoteli ya New Safari, jijini Arusha mwezi Februari.

Kasoro za mchakato wa Katiba mpya zatajwa

ASKOFU DR. BENSON BAGONZA WA DAYOSISI YA KARAGWE

Mpaka Maaskofu wa Kilutheri walipokutana Arusha mwezi Februari, kasoro zifuatazo zimeonekana katika mchakato mzima:

Kasoro ya **kwanza**: Mchakato umejengwa juu ya **nafasi na utashi wa Rais aliye madarakani**. Kwamba, ni yeze mwenye uwezo wa kuamua mambo mengi yanayohusiana na mchakato huu na pili, ni utashi wake umewezesha kuanzishwa kwa mchakato huu. Hii ni kasoro kubwa inayoweza kupotosha mchakato mzima.

Kasoro ya **pili**: **Chama tawala kina sauti kubwa katika mchakato huu**. Hiki ni charma kilichoshiriki kuandika Sheria ya Kuandika Katiba kubwa na hicho ndicho kitakachoandika Katiba hiyo mpya. Historia ya nchi nyngine hailisemei vizuri jumbo hili.

Tatu: **Muda uliotengwa kwa ajili ya mchakato huu ni mfupi** kiasi cha kutishia ubora wake.

Nne: Sheria ya Uandikaji wa Katiba ina upungufu kwa kusema, isipopitishwa na wananchi katika **Kura ya Maoni**, basi Katiba iliyopo inaendelea.

Yaweza kukataliwa katika kipengele kimoja tu na kusababisha Katiba nzima isitumike!

Tano: **Daftari la Wapiga Kura halijaboreshwu**. Matumizi mabaya ya daftari hili ni chimbuko la vurugu katika nchi nyingi zenyen demokrasia changa.

Sita: **Kiwango cha rushwa katika taifa kinatishia uhuru wa watu maskini kufanya uchaguzi jinsi wanavyopenda**. Matajiri wengi na wana siasa wanamiliki vyombo vya habari na wana habari kiasi cha kuwachagulia watu bila utashi wao.

Saba: Kutoptana na ama rushwa au **kukosekana kwa udhibiti wa vyombo vya dola**, hata asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali (civil society), yameishamezwa na mfumo (status quo) na kuwanyima maskini watetezi wazuri. Hata Kanisa halina rekodi nzuri katika kipengele hiki.

Nane: **Kuna mfumo unaonyanyaapaa vyama vya upinzani na viongozi wake**. Wananchi wengi wametishwa na kuuona upinzani kama

uhaini. Hali hii inaweza kuleta madhara makubwa baadaye endapo wanaoitwa wahaini watachukua madaraka na walio madarakani wakaitwa wahaini!

Tisa: Yako maoni yasiyokubaliwa na watawala kuwa **mchakato huu umeanzia mwisho kwenda mwanzo** badala ya kuanzia mwanzo kwenda mwisho. Kwamba, ingelianza kura ya maoni juu ya muungano ndipo Katiba iweze kuandikwa kuliko kuandika Katiba bila kuwa na uhakika kama watu wanaupenda muungano ama la!

HITIMISHO: Uandishi wa Katiba Mpya ni ishara ya kukomaa kwa taifa na kujieleza mbele ya dunia kuptit Katiba yake. Kama ilivyokuwa wakati wa kuandika Katiba ya kupata Uhuru wa bendera, hivi sasa wananchi wengi wanatoa maoni makali kana kwamba wanapambana na mkoloni mwingine. Kimsingi, kilichobadilika ni rangi ya mkoloni, lakini dalili za ukandamizaji wa kimfumo zingali bado zipo. Katiba Mpya inatakiwa kwa sababu maendeleo siku hizi yanapimwa kwa kiwango cha uhuru.

Tanzania ni tunda la itikadi, dini, jinsi na rika zote.


Ashauri kamati kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa iundwe

Askofu Dkt. Heinrich Bedford-Strohm toka Chuo Kikuu cha Bamberg, Ujerumani ambaye ni Profesa Mshauri wa Msuala Mapya ya Theologia, ameshauri Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) liunde kamati ya kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake nchini.

Akitoa mada hivi karibuni kuhusu "Mtazamo wa Kitheolojia kuhusu Umaskini, Mali na Ekolojia", alisema ni kashfa kimaadili kwamba watu 25,000 wanapoteza maisha kila siku duniani kwa maradhi au sababu zinazoweza kuzuulika licha ya kukubalika kimataifa kwa haki za binadamu. Walipojadili mada hiyo maaskofu wa KKKT na kutoka Umoja wa Makanisa ya Kilutheri Ujerumani (VELKD), walisema iko haja kwa taasisi za kiimani kuwa na mipango ya kuhifadhi mazingira hasa kutoptana na kuwepo kwa uchafuzi unaotokana na mifuko ya plastiki.

Walisema "mabadiliko ya hali ya hewa yanayodhahirika kwa ukame, vimbunga na mafuriko yamefanya tuzingatie jinsi ya kufanya shughuli za kiuchumi bila kuendelea kuathiri mahusiano ya kijamii, kitamaduni na kiekolojia."

Pengo la matumizi ya maliasili kati ya nchi tajiri na nchi maskini zinaonesha iko haja ya kuzingatia jinsi gani ya kulinda haki ili kuwa na uchumi endelevu kwa



Askofu Dkt. Heinrich Bedford-Strohm.

manufaa ya vizazi vijavyo.

Uhuru wa soko uwe wa haki kwa kuweka mfumo wa kibiashara inayozuia nchi maskini zisinyonywe na nchi zinazoshirikiana nazo kibiashara.

Askofu Bedford alisema Mashirika ya kiimani (kama KKKT) hayana budi kushiriki katika harakati za kuunda jamii yenye haki kwa kubadilisha mitazamo na mienendo ya waumini wake ili watambue na kuacha utamaduni wa kupenda faida kupita kiasi, matumizi ya anasa na kushindana kulimbikiza mali.

"Ukuaji uchumi usiwe ule wa

kuangamiza mazingira au ekolojia. **Masuala ya uumbaji na mazingira ni masuala ya haki**. Sisi ni sehemu ya uumbaji, hivyo tunapaswa kutumia maliasili bila kuathiri maisha ya viumbe vingine. Tumefikia kiwango cha teknolojia duniani kinachowezesha kuhifadhi mazingira. Hivyo ukuaji kiuchumi uzingatие kuwa na miradi ya maendeleo isiyoathiri uumbaji.

"Biblia inatufundisha Mungu ni wa haki nasi tuwe wa haki kwa kuwa tunamjua Mungu. Na katika kugawana faida hata wale walio pembezoni au maskini wanufaikie na utajiri uliopo kiuchumi. Watu wafanye kazi pamoa na siyo kukinzana.

"Maono kama hayo yanatutaka pia kushirikiana katika ngazi ya kimataifa kwani hakuna mtu anayeweza kuishi peke yake bali wanadamu hutegemeana. Ni muhimu tunapofika katika hatua ya kushirikiana, kuelekeze nguvu katika kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu itokanayo na upепо, hewa, juu, nk.

Hivyo, makanisa na taasisi za kiimani zichukue hatua mahsusni na si kutoa maoni na mahubiri pekee. Kwa pamoa makanisa katika ngazi ya kimataifa yanawajibika kutoa msukumo hadi ufikiwe muafa kuhusu haki katika masuala ya kiuchumi."

Wahitimu Shahada ya Tiba Shufaa

USHIRIKIANO NA VYUO VIKUU

NA TAASISI ZA MAFUNZO:

Kama sehemu ya kukua kwa Kurugenzi ya Afya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kumekuwa na ushirikiano kati Program ya Tiba Shufaa na taasisi za mafunzo kama Chuo Kikuu cha IMTU cha Dar es Salaam ambako wanafunzi wa Stashahada ya uzamili ya Tiba Shufaa -ambayo ni ya kwanza ya aina yake kuanzishwa Tanzania - wamekuwa wakifanya mazoezi ya vitendo katika hospitali za KKKT: Selian na Nkoaranga.

Watumishi wa Kitengo cha Tiba Shufaa Ofisi Kuu ya KKKT, Arusha pia wameshiriki katika kufundisha wanafunzi wa Kozi ya Ushauri wa Kichungaji (Clinical Pastoral Education" - CPE) inayotolewa kila mwaka katika Hospitali ya KCMC, Moshi ambayo inawalenga watumishi wa kiroho wanaoshiriki katika huduma kwa wagonjwa.

USHIRIKI KATIKA MAANDALIZI YA SERA YA TAIFA YA TIBA SHUFAA:

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na wadau wakuu wa tiba shufaa nchini wamekuwa katika mchakato wa kuanda Sera ya Taifa ya Tiba Shufaa (National Policy for Palliative Care Services). Program ya Tiba Shufaa KKKT imeshiriki kwa kiwango kikubwa katika kuchangia utengenezaji wa sera hiyo kama wadau wenye uzoefu wa kutoa huduma hizo. Kwa kushiriki katika maandalizi ya sera hiyo, KKKT imeonyesha jinsi ambavyo mashirika ya kiimani na asasi binafsi zinavyoweza kuchangia katika kuleta mabadiliko chanya kwa manufaa ya wananchi wote.

KUSHIRIKISHA WADAU NA

WAFADHILI MBALIMBALI:

Moja ya changamoto kubwa za tiba shufaa ni ukweli kuwa wagonjwa wengi wa magonjwa ya kusendeka wanaathirika pia kiuchumi kwa sababu ya kuwa



Dkt. Zebadia Paul Mmbando,

Meneja wa Programu ya Huduma ya Tiba Shufaa KKKT. (PICHA KWA HISANI YA DKT. CHRISTOPHER HARTWIG)



© 2014 ELCT PALLIATIVE CARE PROGRAM/ ANNA MAHENGE

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (Kulia), akikabidhi gari lilitolewa na wafadhili wa Palliative Care kutoka College Union Marekani kwa ajili ya Hospitali ya Kilutheri ya Itete, Rungwe.



Mkurugenzi wa Afya KKKT, Dkt. Geoffrey Sigalla (Kushoto), akimkabidhi Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dkt. Salum Sufiani (katikati), vifaa tiba kwa wagonjwa majumbani. Msaada huo ni sehemu ya ufadhili wa watu wa Marekani kupitia Taasisi ya 'AFRICARE'. Mkuu wa Mradi wa KAYA CCI wa AFRICARE, Bi Ranannah Afriye, anasaidia kukabidhi. (© 2014 ELCT PALLIATIVE CARE PROGRAM/ DKT. ZEBADIA MMBANDO)

wagonjwa kwa muda mrefu na hivyo kushindwa kufanya kazi za kuijiingizia kipato. Kwa sababu hii Programu ya Tiba Shufaa KKKT imejenga uhusiano na wafadhili na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kusaidia hospitali za Kanisa pale inapowezekana. Tumefanya kazi na wadau wengi wakiwemo makanisa marafiki kama Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani, Shirika la Misaada la Marekani, "AFRICARE", Chama cha Msalaba Mwekundu, "Pathfinder International" na taasisi 16 za "Palliative & Hospice Care" za Marekani na Ulaya. Misaada mingi huenda katika hospitali lengwa za KKKT kuwanufaisha wagonjwa wanaofikiwa na wataalamu wa vituo hivyo. Misaada hiyo ni magari, madawa, vifaa tiba, kuchangia gharama za watumishi na watoa huduma, nk.

Hivi karibuni pia tumeanzisha uchangiaji wa huduma za Tiba Shufaa kwa baadhi ya wagonjwa katika vituo mbalimbali kwa lengo la kudumisha huduma hii muhimu. Hadi Januari mwaka huu, kitengo kimeweza kuwafikia zaidi ya wagonjwa 15,000 kila mwaka, kazi inayofanyika na watumishi wa afya

walio chini ya hospitali za KKKT kwa kushirikiana na wadau wake. Lakini bado wapo wagonjwa wengi sana wa kansa na magonjwa mengine ya kusendeka ambao hawana uwezo wa kifedha.

HITIMISHO:

Kwa mchango huu, ni wazi kuwa huduma hii imekuwa sana na Kanisa kupitia huduma zake za afya limeendelea kuonyesha uwezo mkubwa katika kumhudumia binadamu kiroho lakini pia kimwili, kijamii na kisaikoloja. Kukua kwa programu hii kumekwenda sambamba na kukua kwa huduma kitaifa katika utoaji huduma, mafunzo, utetezi, kujenga uwezo na uratibishaji ambazo pia ni kazi kuu zinazofanywa na Kurugenzi ya Afya ya KKKT.

Rai kwa Watanzania wenye uwezo wa kiuchumi na **Wasamaria Wema** ambao wangependa kuwasaidia wagonjwa na familia zao wakiwemo watoto yatima na wale wanaoishi na VVU, tunapenda kuwakaribisha ili kuchangia huduma hizo kupitia kitengo hiki.

**Kwa mawasiliano au maswali tuma kwa:
Barua pepe: <mmbandozebs@yahoo.com>**

Simu: 0784 666165

FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

Kila mwaka Washarika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania hukumbuka Siku ya KKKT ambayo mwaka huu itakuwa tarehe 22 Juni 2014. Ifuatayo ni historia fupi kuonesha chimbuko la siku hiyo:

Vyama vilivyoeneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha ‘Berlin III’ au ‘Evangelical Missionary Society for East Africa’ (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

Chama cha pili

Chama cha Misioni cha ‘Berlin I’, nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde (kwa sasa).

Mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya ‘Bethel’. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliama kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia nchini Tanzania mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA, nk. Hakika Neno la Mungu

linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 - 1918 na ya Pili 1939 - 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

Makanisa Saba

Vyama vya misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Na tarehe 23 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana kuunda Kanisa moja la KKKT na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi/Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na ufikapo mwezi Septemba mwaka huu KKKT itakuwa na Dayosisi 24.

Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu amba hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatizo: Misioni na Unjilisti; Mipango na Maendleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ulaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na *kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi* kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT inataasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: 1. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira 2. Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro 3. Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. 4. Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. 5. Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. 6. Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 20 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina

Siku ya KKKT
22 Juni 2014:
Pamoja tujenge
Kanisa la Bwana.

shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng’ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

Kazi za Misioni

KKKT inajihusisha na kazi za misioni ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya maeneo nje ya nchi ni Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi, Uganda na Zambia. Ndani ya nchi maeneo ya misioni ni Tabora, Kigoma na Zanzibar.

Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); ‘Lutheran Mission Cooperation’ (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha “Lutheran Centre”, Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli yenye vitanda 24.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu Mkuu

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

S.L.P. 3033, Arusha

Simu: 250 8856/ 250 8857

Fax 254 8858

Barua pepe: elcthq@elct.or.tz

Tovuti: <http://www.elct.org/>

Au: <http://www.elct.or.tz/>

Upendo FM 107.7



Amani kwa wote

JE UNAFAHAMU KITUO BORA CHA REDIO KATIKATI YA JIJI?

Kwa matangazo ya biashara na mikutano ya Injili,
kwa ushauri wa kiroho na maendeleo ya jamii:
Tangaza kwenye Redio bora ya Upendo na Amani
kwa wote.

Fika sasa **LUTHER HOUSE**

GHOROFYA PILI

SOKOINE DRIVE.

Upendo FM 107.7 Mhz

P.O. Box 13603

Da es Salaam, Tanzania

Simu: 022 212 4228/ 2139556/ 2124221

E-mail: upendofm@yahoo.com

Wakala

Gazeti la Uhuru na Amani
Unapolipa kwa TT NBC; tafadhalii
tuma kivuli cha Pay-in-Slip kwa
Mhariri kwa njia ya Barua Pepe:

<elobulu@elct.or.tz>

A/C ni ile ile: Na: 014103002064



Ifahamu **RADIO SAUTI YA INJILI**

FM 92.2 & 96.2 MHz
MOSHI

RSYI ni rafiki anayekujali kiroho na kimwili.

Katika Masafa ya FM, Radio Sauti ya Injili
kutoka Moshi inasikika vizuri kabisa katika
Masafa yafuatayo:

Moshi	92.2 MHz	Mlalo (Lushoto)	102.6 MHz
Arusha	96.2 MHz	Kisosora (Tanga)	96.7 MHz
Same	100.4 MHz	Morogoro	96.6 MHz
Kibaya (Kiteto)	102.9 MHz	Hakwe (Rombo)	96.4 MHz

Aidha Radio Sauti ya Injili, Moshi inasikika kwenye tovuti
dunia nzima kwa saa 24 www.sautiyainjili.org

Radio Sauti ya Injili inatangaza vipindi
mbalimbali vikiwemo vya maendeleo, afya,
uchumi, habari na halikadhalika vipindi vya
mafundisho ya dini. Unaweza kupata habari
moto moto za kitaifa na kimataifa katika kipindi
cha Dira ya Leo.

Wasiliana na:

Mkurugenzi RSYI

S.L.P. 777, Moshi

Simu: 027 27 52772 au 027 27 53080

E-mail: redio@elct.org

Tovuti: www.sautiyainjili.org

Kumbuka kuwa RSYI ipo kwa ajili yako. Aidha, kijamii.
Endelea kuimarisha huduma nzuri hii kwa hali na mali.

Radio Furaha **96.7 FM**

**Sikiliza matangazo ya
kituo bora cha Redio Iringa
na maeneo jirani.**

Kwa maoni, ushauri wa kiroho
na kijamii wasiliana na:

Meneja: Protas Kanemela

Simu: +26 27 003 43

Fax: +255 262 701 198

Barua pepe: elctrdr1987@yahoo.com

Lutheran Uhuru Hotel and Conference Centre



Mandhari ya Kuvutia



Malazi Safi



Nyamachoma Maarufu



Vyakula vya Kikwetu na Kigeni

Kwa Mikutano, Semina, Harusi, Malazi, Mapumziko na Nyamachoma
Pia Tunapeleka Wageni Mlima Kilimanjaro na Mbuga za Wanyama

Ukihitaji Maelezo Zaidi, Wasiliana na Meneja

Lutheran Uhuru Hotel & Conference Centre

P.O. Box 1320, Moshi, Tanzania: Simu: +255 272 754 084; +255 753 037 216
e-mail: reservation@uhuruhotel.org; manager@uhuruhotel.org
www.uhuruhotel.org

Huduma za Uchapishaji

Moshi Lutheran Printing Press ni kiwanda chako cha uchapishaji kinachoongoza kote kaskazini ya Tanzania kuhusu ubora, unafuu wa gharama, kasi na uaminifu. Tunachapisha:-

Vitabu, Kadi za kila aina, Majorida na Magazeti, Mabango, Vipeperushi, Bahasha, Hati za Fedha, Tikiti, Ratiba, Pakiti, Majalada, Daftari, n.k.

Tunatoa huduma kamili za typesetting na usanifu.

Tunakarabati vitabu vichakavu vikawa vipyta tena.

Kwetu hakuna kazi iliyo ndogo mno au kubwa mno.

Tunakushauri kuhusu kufanikisha malengo yako.

Fika Mara Moja

MOSHI LUTHERAN PRINTING PRESS

S.L.P 301, MOSHI, Simu: +255 272 750 546

E-mail: lutheranpress@yahoo.com